BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA KUMI NA MOJA LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA TATU

Kikao cha Thelathini na Saba – Tarehe 23 Juni, 2026

Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua Zitasomwa.

## I. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

**Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi:**

Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Uvuvi, Nam. 7 ya 2010 na Kutunga Sheria ya Mamlaka ya Maendeleo ya Uvuvi na Uhifadhi wa Bahari kwa ajili ya Kusimamia, Kuendeleza Uvuvi na Kuhifadhi Maliasili za Bahari na Kuweka Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo.

**Waziri wa Habari, Sanaa, Utamaduni na Michezo:**

Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya kuanzisha Shirika la Magezeti ya Serikali, Nam. 11 ya 2008 na Kutunga upya Sheria ya Shirika la Magazeti Zanzibar kwa madhumuni ya kuendesha Biashara ya Magazeti na Kuweka Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo.

**Mwenyekiti wa Kamati ya Kanuni na Sheria Ndogo:**

Azimio la Marekebisho ya Kanuni za Kudumu za Baraza la Wawakilishi, Toleo la 2024.

## II. MASWALI:

### Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:

340 MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (Jimbo la Paje) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:

Pamoja na umuhimu wa Waheshimiwa Mawaziri kwa wananchi wanaowahudumia kuna tabia ya baadhi yao kuzima simu zao wanapopigiwa na wananchi hao hali inayosababisha wananchi kukosa fursa ya kueleza matatizo yao lakini pia kunawakosesha Mawaziri hao haki ya kupata taarifa sahihi ya matatizo yanayowakabili wananchi wao.

(a) Kwa nini baadhi ya Mawaziri wanafunga simu na kujifanya kuwa hawapatikani.

(b) Kwa kufanya hivyo, hawaoni kuwa wanakwepa majukumu yao na kuwakatisha tamaa wananchi waliowatuma.

397. MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (Jimbo la Paje) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:

Hivi karibuni katika nchi yetu kumezuka uvumi ulioanzia Tanzania bara, ikidaiwa kuwa wapo watu wanawashika bega wanaume na sehemu zao za siri zinapotea. Uvumi huu umeleta taharuki, hofu, wasiwasi sana katika jamii na kusababisha madhara makubwa na baadhi ya watu kupigwa na mmoja kuripotiwa kuuwawa.

(a) Kwa nini Serikali ilichelewa kuchukuwa hatua za haraka kupiga marufuku kuenezwa kwa taharuki hiyo mpaka madhara makubwa yametokea.

(b) Kwa kuwa matukio ya taharuki kama hizi hujitokeza kila baada ya miaka fulani, kuanzia na hadithi za popobawa na mengine ambazo huleta madhara hayo hayo ya watu kujeruhiwa na kuuwawa. Je, Serikali kupitia wataalamu wa masuala ya kijamii imefanya utafiti kujuwa chanzo chake ili kuweza kudhibiti na kuepusha madhara ya matukio hayo.

(c) Kwa kuwa kuna baadhi ya vyombo vya habari na Mitandao ya Kijamii iliyoonekana kushabikia na kueneza taharuki hii kwa namna moja au nyengine, ni hatua gani za kisheria zimechukuliwa na Serikali dhidi ya vyombo hivyo.

470. MHESHIMIWA KOMBO MWINYI SHEHE (Jimbo la Wingwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:

Kwa kuwa ndani ya visiwa vyetu vya Unguja na Pemba kumejitokeza wimbi la upoteaji wa watu na hasa vijana katika mazingira ya utatanishi. Na kwa kuwa upoteaji huu wa watu unaleta taharuki kubwa kwa jamii na kupelekea wananchi kuwa na khofu kila wanapotembea.

(a) Je, Serikali inalitambua vipi jambo hili.

(b) Ni ipi kauli ya Serikali kuhusiana na kadhia hii nzito inayoendelea.

(c) Je, Serikali inayatambua ni matukio mangapi ya upotevu wa watu yamejitokeza hadi sasa.

## <u>Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale:</u>

91. MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (Jimbo la Paje) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale:

Kumekuwa na udhibiti wa wafanyabishara wadogo wadogo katika maeneo ya Mji Mkongwe pamoja na wananchi wanaoegesha vyombo vyao vya moto katika maeneo hayo. Wananchi hao wanapokamatwa wanalipishwa viwango vikubwa vya faini za papo kwa papo.

(a) Je, viwango vya faini hizo wanazolipishwa vinatozwa kwa sheria au kanuni ipi. Na vipi Kanuni hiyo imepitiwa na Kamati ya Kanuni na Sheria Ndogo ya Baraza la Wawakilishi.

(b) Je, wananchi wanaotozwa faini hizo za papo kwa papo wanapatiwa risiti, ili kuthibitisha kuwa faini hizo zinaenda Serikalini.

(c) Je, ni kiasi gani cha fedha za faini za papo kwa papo ambacho kimepatikana katika kipindi cha mwaka huu wa fedha 2025/26.

107. MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (Jimbo la Paje) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale:

Mamlaka ya Mji Mkongwe kwa kipindi kirefu imejivunia kuwa na wataalamu wa fani za uhandisi, ambao walikuwa wanaufahamu vizuri sana Mji Mkongwe. Hata hivyo, wataalamu hao wote wameondoshwa na hivi sasa wameletwa wengine ambao hawana

ufahamu wa kutosha wa uhifadhi na uendelezaji wa Mji Mkongwe.

(a) Je, ni sababu gani za msingi zilizopelekea wataalamu hao kuondoshwa wote.

(b) Kwa nini Serikali haioni kuwa kuondoshwa kwa wataalamu hawa wote wenye uzoefu mkubwa na Mji Mkongwe, ni hatua za kuhujumu hifadhi na uendelezaji wa Mji Mkongwe ambao ni urithi pekee wa Kimataifa kwa Zanzibar.

<u>**Wizara ya Mawasiliano, Teknolojia ya Habari na Ubunifu:**</u>

184. MHESHIMIWA MAHMOUD SHINENI ALI (Jimbo la Chambani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano, Teknolojia ya Habari na Ubunifu:

Uweledi kazini ni jambo muhimu sana katika utendaji wa kazi yoyote ingawa hivi sasa kumeibuka changamoto kubwa kwa baadhi ya wahudumu wa sekta binafsi na watumishi wa Serikalini kuchukua matukio ya picha au picha mjongeo (video), zinazoonesha baadhi ya matukio ya wananchi wanapofika kupata huduma au inapotokea dharura wakiwa katika hali mbaya. Jambo hili linaenda kinyume na sheria za nchi na taratibu za faragha za kurikodi na kutoa picha au video bila ya ridhaa ya muhusika.

(a) Je, Serikali imelifanyia tathmini jambo hili na itachukua hatua gani kwa wale wote wanaovunja miiko ya uweledi kazini.

(b) Kesi ngapi zimesharipotiwa kwa kipindi cha 2020-2026 na hatua gani zimechukuliwa na Serikali.

(c) Kwa nini Serikali isianzishe mfumo rasmi wa kudhibiti matumizi ya vifaa vya kieletroniki kwenye Ofisi za Umma.

459. MHESHIMIWA JUMA HASSAN THABIT (Jimbo la Fuoni) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano, Teknolojia ya Habari na Ubunifu:

Serikali imetumia gharama kubwa katika uwekezaji wa mifumo ili kupunguza upotevu wa mapato.

Ni hatua zipi Serikali imechukua kwa baadhi ya taasisi na mashirika yanayofanya baadhi ya malipo bila ya kutumia mfumo.

## III. HOJA ZA SERIKALI:

### Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi:

Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Uvuvi, Nam. 7 ya 2010 na Kutunga Sheria ya Mamlaka ya Maendeleo ya Uvuvi na Uhifadhi wa Bahari kwa ajili ya Kusimamia, Kuendeleza Uvuvi na Kuhifadhi Maliasili za Bahari na Kuweka Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo – Kusomwa kwa Mara ya Kwanza.

### Waziri wa Habari, Sanaa, Utamaduni na Michezo:

Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Kuanzisha Shirika la Magezeti ya Serikali, Nam. 11 ya 2008 na Kutunga upya Sheria ya Shirika la Magazeti Zanzibar kwa madhumuni ya kuendesha Biashara ya Magazeti na Kuweka Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo - Kusomwa kwa Mara ya Kwanza.

## IV. HOJA ZA KAMATI :

### Mwenyekiti wa Kamati ya Kanuni na Sheria Ndogo:

Azimio la Marekebisho ya Kanun iza Kudumu za Baraza la Wawakilishi, Toleo la 2024.



Zanzibar,
23 Juni, 2026.

(Raya Issa Msellem)
KATIBU WA BARAZA LA
WAWAKILISHI, ZANZIBAR.